JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2021

KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2021

KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P.2624,
Dar es Salaam. Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI iv

1.0 UTANGULIZI 1

1.1 SEHEMU A: Kusikiliza, Lugha ya Kifasihi na Sarufi 2

1.2 SEHEMU B: Utungaji..... 54

1.3 SEHEMU C: Ufahamu 58

2.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI 67

3.0 HITIMISHO 69

4.0 MAPENDEKEZO 69

KIAMBATISHO CHA PEKEE..... 71

DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Kiswahili mwaka 2021. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa watunga sera, wathibiti ubora wa shule, walimu, wanafunzi, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu umahiri walionao wanafunzi katika kujibu maswali na changamoto zilizowakabili.

Aidha, taarifa hii imeonesha mambo mbalimbali yaliyochangia watahiniwa kujibu maswali kwa usahihi. Mambo hayo ni pamoja na kuelewa matakwa ya swali pamoja na kuwa na maarifa ya kutosha katika umahiri wa aina mbalimbali katika somo la Kiswahili. Usahihi wa majibu yaliyotolewa na watahiniwa unadhihirisha kwamba ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili ulifanyika vizuri. Hata hivyo zipo sababu za watahiniwa kushindwa kujibu maswali kwa usahihi ikiwa ni pamoja na kushindwa kutambua matakwa ya swali, kuchagua jibu zaidi ya moja katika kujibu maswali mbalimbali kinyume na maelekezo. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila swali umeainishwa katika uchambuzi huu kwa kutumia maelezo, jedwali na vielelezo.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kutafuta mbinu stahiki na kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki ipasavyo katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Kiswahili ulikuwa na maswali arobaini na tano (45). Maswali arobaini (40) yalikuwa ya kuchagua jibu sahihi na kila swali lilikuwa na alama moja (1). Maswali hayo yaligawanywa katika sehemu A, B na C. Sehemu A ilikuwa na alama thelethini na tano (35) sehemu B ilikuwa na alama tano (5). Aidha, kulikuwa na maswali matano (5) ya kujieleza kutoka sehemu C (Ufahamu) ambayo yalikuwa na alama mbili (2) kwa kila swali.

Jumla ya watahiniwa 1,132,084 walisajiliwa kufanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2021 kwa somo la Kiswahili. Waliofanya mtihani walikuwa 1,107,775. Watahiniwa waliofaulu mtihani huu ni 979,877 sawa na asilimia 88.50.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umefanyika kwa kuchambua maswali yote ya mtihani, yaani maswali ya kuchagua herufi ya jibu sahihi na kutoa majibu mafupi. Uchambuzi wa takwimu umewasilishwa kwa njia ya jedwali kwa kubainisha asilimia ya watahiniwa waliochagua kila chaguo kwa kila swali, katika swali la 1 - 40 na asilimia ya watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali la 41 - 45. Aidha, vielelezo vimetumika katika uchambuzi wa maswali ya majibu mafupi kwa lengo la kuonesha umahiri wa watahiniwa na changamoto walizokuwa nazo. Rangi mbalimbali zimetumika kuonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya watahiniwa kwa kila swali. Rangi nyekundu imetumika kuwakilisha kiwango hafifu cha ufaulu yaani 0 – 39. Rangi ya njano imetumika kuwakilisha kiwango cha wastani cha ufaulu, yaani asilimia 40 – 59 na rangi ya kijani imetumika kuwakilisha kiwango kizuri cha ufaulu, yaani asilimia 60 – 100**.** Aidha, alama ***** imetumika katika jedwali na vielelezo kuonesha jibu sahihi kwa

kila swali. Vilevile, watahiniwa waliochagua jibu zaidi ya moja au hawakuchagua chaguo lolote imeoneshwa kwa neno “mengine”.

1.1 SEHEMU A: Kusikiliza, Lugha ya Kifasihi na Sarufi

Sehemu hii ilikuwa na maswali thelathini na tano (35). Swali la kwanza hadi la tano (1-5) yalipima umahiri wa mtahiniwa kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza. Swali la sita (06) hadi thelathini na tano (35) yalipima umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali, kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma na kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali. Watahiniwa walisomewa hadithi ifuatayo:

Katika kujibu swali la 1- 5, watahiiwa walitakiwa kusikiliza hadithi waliyosomewa kisha wachague herufi ya jibu sahihi katika swali la 1 hadi la 5. Hadithi ilikuwa kama ifuatavyo:

Hapo zamani za kale kulikuwa na kijiji kimoja kilichomilikiwa na Nyuki. Kijiji kiliongozwa na Malkia wa Nyuki. Malkia alikuwa analindwa na askari hodari. Pia alikuwa na vibaraka waliotumika kupeleka habari mbalimbali katika vijiji vya jirani. Malkia wa nyuki alikuwa hapendi kuwa na wanakijiji hohehahe. Muda mwingi aliwasisitiza wafanye kazi kwa bidii. Nyuki wengine walionekana wakiingia na kutoka kwenye mzinga muda wote. Wafanyakazi wengine walijizatiti katika kutafuta nekta kwenye maua.

Malkia alihakikisha nyuki wote wanatekeleza wajibu wao bila shuruti. Aliamini umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Aliuza asali nyingi sana na kupata utajiri mwingi. Aliwafundisha wanakijiji wake wimbo wa umoja na ushirikiano katika maendeleo, wakawa wanauimba kila

mara. Wanakijiji walijawa na bashasha na furaha muda wote kutokana na mafanikio yao.

Swali la 1: Malkia wa nyuki alikuwa analindwa na nani?

A Vibaraka

B Askari hodari

C Wanakijiji

D Nyuki Hohehahe

E Wafanyakazi

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Kielelezo Na. 1 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Kielelezo Na. 1*: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.*

Kielelezo Na. 1 kinaonesha kuwa watahiniwa 1,014,584 sawa na asilimia 91.59 walichagua jibu sahihi B *Askari hodari*. Watahiniwa hao walielewa kuwa askari hodari ndio waliokuwa walinzi wa Malkia wa nyuki.

Hata hivyo, watahiniwa 82,719 sawa na asilimia 7.5 walichagua kati ya vipotoshi A *vibaraka, C wanakijiji, D Nyuki hohehahe, E Wafanyakazi*. Waliochagua kipotoshi *vibaraka* walishindwa kuelewa kuwa vibaraka walitumika kupeleka habari vijiji vya jirani na si kumlinda Malkia. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *wanakijiji* walishindwa kuelewa kuwa wanakijiji ni wale nyuki wote walioongozwa na malkia wa nyuki. Aidha, waliochagua kipotoshi *nyuki hohehahe* hawakuwa sahihi kwa kuwa nyuki hohehahe walikuwa hawapendwi na Malkia wa nyuki kwa sababu hawafanyi kazi kwa bidii. Pia, uteuzi wa kipotoshi *wafanyakazi* haukuwa sahihi kwani wafanyakazi walikuwa wanatafuta nekta kwenye maua na si kumlinda malkia wa nyuki. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na umahiri wa kusikiliza na kuelewa hadithi waliyosomewa.

Swali la 2: Ni kitu gani ambacho malkia wa nyuki hakukipenda?

A Wanakijiji hohehahe
B Mafundi wa masega
C Ushirikiano wa nyuki
D Vibaraka wa malkia
E Kuwalipa vibarua

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri sana. Kielelezo Na. 2 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Kielelezo Na. 2: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.*

Kielelezo Na. 2 kinaonesha kuwa watahiniwa 996,857 sawa na asilimia 89.9 walichagua jibu sahihi A *wanakijiji hohehahe*. Watahiniwa hao walionesha umahiri wa kuweza kutambua kuwa, Malkia wa Nyuki hakupenda wanakijiji hohehahe wasiofanyakazi kwa bidii.

Hata hivyo, watahiniwa 100,803 sawa na asilimia 10.0 walichagua kati ya vipotoshi B *mafundi wa masega, C ushirikiano wa nyuki, D* vibaraka *wa malkia, E kuwalipa vibarua.* Watahiniwa waliochagua *mafundi wa masega* hawakuwa sahihi kwa sababu mafundi wa masega hawakutajwa katika hadithi waliyosomewa. Vilevile, uteuzi wa kipotoshi *ushirikiano wa nyuki* haukuwa sahihi kwani malkia wa nyuki alikuwa akipenda ushirikiano na si kinyume chake. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *vibaraka wa malkia* haukuwa sahihi kwani vibaraka wa malkia walipendwa na malkia kwa kuwa ndio waliotumika kupeleka habari vijiji vya jirani. Vilevile, waliochagua kipotoshi *kuwalipa vibarua* walishindwa kuelewa maudhui ya hadithi waliyosomewa.

Swali la 3: Nani alijishughulisha kutafuta nekta kwenye maua?

A Nyuki wote

B Vibarua

C Wafanyakazi

D Vibaraka

E Wanakijiji

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 1 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 1: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	303,514	35,406	596,504	71,417	88,378	12,556
Asilimia ya Watahiniwa	27.4	3.2	53.8	6.4	8.0	1.1

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa watahiniwa 596,504 sawa na asilimia 53.8 walichagua jibu sahihi C *wafanyakazi*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kusikiliza na kuelewa maudhuli yaliyomo kwenye hadithi waliyosomewa na msimamizi hivyo kuweza kuelewa kuwa wafanyakazi ndio waliojishughulisha kutafuta nekta kwenye maua.

Hata hivyo, watahiniwa 498,710 sawa na asilimia 45.0 walichagua vipotoshi A *nyuki wote*, B *vibarua,* D *vibaraka*, na E *wanakijiji*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *nyuki wot*e walishindwa kuelewa kuwa shughuli ya kutafuta nekta ilifanywa na baadhi ya nyuki na siyo nyuki wote. Vilevile, waliochagua kipotoshi B *vibarua* walishindwa kuelewa maudhui ya hadithi waliyosomewa kwani vibarua hawakuhusika kutafuta nekta kwenye maua. Pia, waliochagua kipotoshi *vibaraka*

walivutiwa na jibu hili kutokana na kufananisha shughuli za wafanyakazi na vibaraka. Aidha, waliochagua Kipotoshi *wanakijiji,* walishindwa kuelewa kuwa wanakijiji ni nyuki wote waliokuwa wakiongozwa na malkia wa nyuki.

Swali la 4: Utajiri katika kijiji cha nyuki ulitokana na nini?

A Kuuza asali

B Kuuza nta

C Kuuza masega

D Kuuza maua

E Kuuza mizinga

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Kielelezo Na. 3 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Kielelezo Na. 3*: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo*

Kielelezo Na. 3 kinaonesha kuwa, watahiniwa 1,005,029 sawa na asilimia 90.7 walichagua jibu sahihi A *kuuza asali.* Hivyo, walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusikiliza na kuelewa maudhui yaliyomo kwenye hadithi waliyosikiliza.

Hata hivyo, watahiniwa 92,108 sawa na asilimia 8.3 walichagua vipotoshi B *kuuza nta, C kuuza masega, D kuuza* maua*, E kuuza mizinga.* Waliochagua kipotoshi *kuuza nta* walivutiwa na jibu hili kutokana na kuelewa kuwa nta ni mojawapo ya mazao ya nyuki lakini katika hadithi, utajiri katika kijiji cha nyuki ulitokana na asali na si uuzaji wa nta. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *kuuza masega* walishindwa kuelewa kuwa masega ni nyumba ya nyuki iliyotengenezwa kwa nta na hutumika kuhifadhi asali na watoto wa nyuki. Maudhui ya hadithi hayakuonesha kuwa biashara ya masega ndiyo iliyoleta utajiri katika kijiji cha nyuki. Pia, waliochagua kipotoshi *kuuza maua* hawakuwa sahihi kwa sababu uuzaji wa maua haukubainishwa katika hadithi waliyosomewa. Waliochagua kipotoshi hiki walivutiwa na jibu hili kutokana na nyuki kuonekana wakirukaruka kwenye maua kwa ajili ya kuchukuwa nta. Pia, waliochagua kipotoshi *kuuza mizinga* walishindwa kuelewa maudhui ya hadithi waliyosomewa na msimamizi. Aidha, watahiniwa hao walivutiwa na jibu hili kwa kuwa mizinga hutumika kufugia nyuki.

Swali la 5: Nani walitumika kupeleka habari mbalimbali katika vijiji vya jirani?

A Vibarua

B Wafanyakazi

C Vibaraka

D Wanakijiji

E Nyuki

Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 2 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 2: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	63,312	78,494	752,626	109,394	92,313	11,636
Asilimia ya Watahiniwa	5.7	7.1	67.9	9.9	8.3	1.1

Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa watahiniwa 752,626 sawa na asilimia 67.9 walichagua jibu sahihi C *vibaraka*. Watahiniwa hao waliweza kuelewa maudhui yaliyomo katika hadithi waliyosomewa, hivyo kuweza kujibu swali hili.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 343,513 sawa na asilimia 31.0 walichagua vipotoshi A *vibarua, B wafanyakazi, D wanakijiji* na *E nyuki.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *vibarua* walishindwa kutofautisha neno vibarua na vibaraka kutokana na kutosikiliza kwa makini hadithi waliyosomewa na msimamizi. Pia, waliochagua kipotoshi *wafanyakazi* walishindwa kuelewa kuwa, wafanyakazi wengi walijishughulisha na kutafuta nekta kwenye maua na si kupeleka habari

katika vijiji vya jirani. Aidha, waliochagua kipotoshi *wanakijiji* walishindwa kuelewa kuwa wanakijiji walikuwa ni nyuki wote waliokuwa wanaongozwa na malkia wa nyuki. Watahiniwa waliochagua jibu hili walivutiwa na maneno yaliyokuwa kwenye swali ambayo ni *vijiji vya jirani*.

Vilevile, waliochagua kipotoshi *nyuki* hawakuelewa hadithi waliyosomewa. Hata hivyo, walivutiwa na jibu hilo kwa sababu waliojishughulisha na kupeleka habari mbalimbali katika vijiji vya jirani ni vibaraka ambao ni miongoni mwa nyuki. Hivyo, hawakuelewa kuwa nyuki waligawanywa katika makundi mbalimbali kutokana na kazi zao ili kukuza ushirikiano katika jamii yao.

Swali la 6: Walifanya juu chini ili kuleta maendeleo katika kijiji chao. Nahau "fanya juu chini" inafafanuliwa na kifungu kipi cha maneno kati ya vifuatavyo?

A Walijitahidi kwa kila njia.
B Walishirikiana kwa pamoja.
C Walijituma kwa ujasiri.
D Walijituma kwa uzalendo.
E Walitumia nguvu.

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kueleza maana ya nahau na kuzitumia katika mazungumzo kwa kuzingatia miktadha mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 3 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 3: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	761,641	209,532	43,973	39,652	39,904	13,073
Asilimia ya Watahiniwa	68.8	18.9	4.0	3.6	3.6	1.2

Jedwali Na. 3 linaonesha kuwa watahiniwa 761,641 sawa na asilimia 68.8 walichagua jibu sahihi A *walijitahidi kwa kila njia.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika matumizi na maana ya nahau *fanya juu chini .*

Hata hivyo, watahiniwa 333,061 sawa na asilimia 30.1 walichagua vipotoshi B *walishirikiana kwa pamoja,* C *walijituma kwa ujasiri*, D *walijituma kwa uzalendo* na E *walitumia nguvu*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *walishirikiana kwa pamoja* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hicho ni cha nahau *bega kwa bega* hivyo halikuwa jibu sahihi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *walijituma kwa ujasiri* hawakuelewa kuwa ni kufanya kazi kwa moyo au kujituma bila woga. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *walijituma kwa uzalendo,* likiwa na maana ya kuipenda, kuitumikia na kuitetea nchi yako. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *walitumia nguvu* walishindwa kuelewa kuwa kifungu hicho cha maneno kinaendana na nahau tumia mabavu.

Swali la 7: Nahau ipi yenye maana ya “kunywa pombe?”

A Piga mbizi

B Piga chenga

C Piga yowe

D Piga soga

E Piga maji

Swali hili lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kueleza maana za nahau kwa kuzingatia miktadha mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 4 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 4: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C	D	E*	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	103,185	66,282	80,391	65,587	779,126	13,204
Asilimia ya Watahiniwa	9.3	6.0	7.3	5.9	70.3	1.2

Jedwali Na. 4 linaonesha kuwa watahiniwa 779,126 sawa na asilimia 70.3 walichagua jibu sahihi E *piga maji* lenye maana kunywa pombe. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu nahau hivyo kuweza kuchagua jibu sahihi.

Watahiniwa 315,445 sawa na asilimia 28.5 walichagua kati ya vipotoshi A *piga mbizi* B *piga chenga* C *piga yowe* D *piga soga*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *piga mbizi* walishindwa kuelewa kuwa nahau hiyo ina maana ya kuzama au kuogelea majini. Waliochagua kipotoshi *piga chenga* walishindwa kuelewa kuwa nahau hiyo maana yake ni kukwepa kwa ujanja. Waliochagua *piga yowe* walishindwa kuelewa kuwa maana yake ni kutoa kelele au sauti kubwa. Aidha, waliochagua kipotoshi piga soga walishindwa kuelewa kuwa maana yake ni mazungumzo au maongezi.

Katika swali la 8 hadi la 34 yalihusu umahiri mahususi wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali, kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali na kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali.

Swali la 8: Katika sentensi "Dada alimwambia kuwa atakapopata muda atakuja nyumbani," mzungumzaji ametumia nafsi gani kati ya hizi?

A Nafsi ya pili wingi

B Nafsi ya tatu wingi

C Nafsi ya tatu umoja

D Nafsi ya pili umoja

E Nafsi ya kwanza wingi

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kutumia nafsi katika sentensi kwa kuzingatia hali ya umoja na wingi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu. Jedwali Na. 5 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 5: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	136,669	110,984	436,192	276,320	133,531	14,079
Asilimia ya Watahiniwa	12.3	10.0	39.4	24.9	12.1	1.3

Jedwali Na. 5 linaonesha kuwa, watahiniwa 657,504 sawa na asilimia 59.3 walichagua vipotoshi A *nafsi ya pili wingi*, B *nafsi ya tatu wingi*, D *nafsi ya pili umoja* na E *nafsi ya kwanza wingi*. Watahiniwa waliochagua

kipotoshi *nafsi ya pili wingi* ambacho ni *ninyi* walishindwa kuelewa kuwa kiambishi chake ni *m*- ambacho hutokea katika vitenzi vinavyounda sentensi. Vilevile, uteuzi wa kipotoshi *nafsi ya tatu wingi* unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa nafsi ya tatu wingi ni *wao* na kiambishi chake ni *wa*- ambacho hutokea katika vitenzi vinavyounda sentensi.

Uteuzi wa kipotoshi *nafsi ya pili umoja* ambacho ni *wewe* unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa nafsi hiyo huwakilishwa na kiambishi awali *u*- katika vitenzi. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *nafsi ya kwanza wingi* ambacho ni *sisi*, watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa nafsi hiyo huwakilishwa na kiambishi awali *tu*- katika vitenzi. Kwa ujumla watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kutumia nafsi katika sentensi.

Hata hivyo, watahiniwa 436,192 sawa na asilimia 39.4 walichagua jibu sahihi C *nafsi ya tatu umoja*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kutumia nafsi na viambishi vyake. Hivyo waliweza kutambua kuwa sentensi hii ina kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja ambacho ni *yeye* kikiwakilishwa na kiambishi awali *a*- katika neno *atakapopata* na neno *atakuja*.

Swali la 9: “Sisi ni wanafunzi hodari wa somo la Kiswahili.” Kauli hiyo inawakilisha nafsi ipi kati ya hizi zifuatazo?

A Nafsi ya kwanza umoja

B Nafsi ya tatu wingi

C Nafsi ya tatu umoja

D Nafsi ya kwanza wingi

E Nafsi ya pili wingi

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kutumia nafsi katika sentensi kwa kuzingatia hali ya umoja na wingi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 6 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 6: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C	D*	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	127,989	145,352	85,884	521,503	212,156	14,891
Asilimia ya Watahiniwa	11.6	13.1	7.8	47.1	19.2	1.3

Jedwali Na. 6 linaonesha kuwa, watahiniwa 521,503 sawa na asilimia 47.1 walichagua jibu sahihi D *nafsi ya kwanza wingi*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kutumia nafsi katika sentensi, hivyo waliweza kubaini kuwa kauli hiyo inawakilisha nafsi ya kwanza wingi iliyobainishwa na neno *sisi.*

Watahiniwa 571,379 sawa na asilimia 51.6 walichagua kati ya vipotoshi A *nafsi ya kwanza umoja*, B *nafsi ya tatu wingi* C *nafsi ya tatu umoja* na E *nafsi ya pili wingi*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *nafsi ya kwanza umoja* walishindwa kuelewa kuwa nafsi ya kwanza umoja ni *mimi.* Uteuzi wa kipotoshi nafsi ya tatu wingi ulitokana na watahiniwa kushindwa kuelewa kuwa nafsi ya tatu wingi ni *wao*. Uteuzi wa kipotoshi *nafsi ya tatu umoja* unatokana na watahiniwa kushindwa kuelewa kuwa kiwakilishi nafsi ya tatu umoja ni *yeye.* Uteuzi wa kipotoshi nafsi ya pili wingi unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa kiwakilishi cha nafsi ya pili wingi ni ninyi au nyinyi. Uteuzi wa vipotoshi hivyo

unathibitisha kuwa watahiniwa hao hawana umahiri wa kutosha katika kutumia nafsi kwa kuzingatia hali ya umoja na wingi.

Swali la 10: “Daktari alisema kwamba mgonjwa wetu amepata ahueni.’’
Hiyo ni aina gani ya kauli kati ya zifuatazo?

A Tata

B Mazoea

C Halisi

D Taarifa

E Kutenda

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kutunga sentensi kwa kutumia kauli taarifa. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 7 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 7: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C	D*	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	49,757	53,503	170,406	781,071	40,824	12,214
Asilimia ya Watahiniwa	4.5	4.8	15.4	70.5	3.7	1.1

Jedwali Na. 7 linaonesha kuwa, watahiniwa 781,071 sawa na asilimia 70.5 walichagua jibu sahihi D *taarifa.* Watahiniwa hao, walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kauli mbalimbali ambapo waliweza kubaini kuwa sentensi hiyo ipo katika kauli taarifa, yenye kuonesha kuwa yalikuwa mazungumzo au maelezo ya mtu mwingine kwa kuwa na maneno “alisema kwamba”.

Watahiniwa 314,470 sawa na asilimia 28.4 walichagua kati ya vipotoshi A *tata*, B *mazoea*, C *halisi* na E *kutenda*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *tata* walishindwa kubaini kuwa ni aina ya tungo au sentensi yenye maana zaidi ya moja. Uteuzi wa kipotoshi *mazoea* ulisababishwa na watahiniwa kutokuelewa kuwa hali ya *mazoea* ni hali ya utendekaji wa jambo na huwakilishwa na kiambishi *hu* katika kitenzi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *halisi* walishindwa kubaini kuwa kauli halisi hutoka moja kwa moja kwa msemaji. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *kutenda* unaonesha kuwa watahiniwa hawana uelewa kuwa kutenda ni mojawapo ya kauli za utendaji..

Swali la 11: Masumbuko aliwaambia kuwa, hataingia darasani tena. Kauli halisi ya sentensi hii ni ipi kati ya zifuatazo?

A Masumbuko aliwaambia kuwa, “haingii darasani tena.”

B Masumbuko aliwaambia, “hataingia darasani tena.”

C Masumbuko aliwaambia, “sitaingia darasani tena.”

D Masumbuko aliwaambia, “hakuingia darasani tena.”

E Masumbuko aliwaambia “kamwe haingii darasani.”

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kutumia kauli halisi katika Lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 8 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 8: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	174,414	254,990	568,036	40,873	55,681	13,781
Asilimia ya Watahiniwa	15.7	23.0	51.3	3.7	5.0	1.2

Jedwali Na. 8 linaonesha kuwa, watahiniwa 568,036 sawa na asilimia 51.3 walichagua jibu sahihi C "*Masumbuko aliwaambia," sitaingia darasani tena."* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kauli halisi yenye kuonesha kuwa ni mazungumzo au maelezo kutoka kwa mtu mwenyewe na si taarifa toka kwa mtu mwingine hasa kwa kuwepo kwa kiambishi *si-* kinachorejelea mtenda katika kitenzi *sitaingia* kwenye swali husika.

Watahiniwa 525,958 sawa na asilimia 47.5 waliochagua kati ya vipotoshi A *Masumbuko aliwaambia kuwa," haingii darasani tena,"* B *Masumbuko aliwaambia*, "*hataingia darasani tena,"* D Masumbuko, "aliwaambia hakuingia darasani tena," na E *Masumbuko aliwaambia," kamwe haingii darasani."* Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walishindwa kuelewa kuwa vyote huelezea kauli taarifa na si kauli halisi. Vipotoshi hivyo vina viambishi vinavyotoa taarifa ya mtu mwingine, kama vile, **ha-i** katika neno *haingii*, **ha-ta** katika neno *hataingia*, **ha-ku** katika neno *hakuingia*.

Swali la 12: “Nyamante alikata shauri na kuwaambia wenzake, kweli elimu ndiyo mkombozi wa mtoto wa kike.” Nahau “kata shauri” katika sentensi hii ina maana ipi kati ya zifuatazo?

A Kuamua
B Kuwatahadharisha
C Kuwaasa
D Kuonya
E Kufundisha

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kueleza maana za nahau mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 9 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 9: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	528,365	162,781	218,363	105,755	77,392	15,119
Asilimia ya Watahiniwa	47.7	14.7	19.7	9.5	7.0	1.4

Jedwali Na. 9 linaonesha kuwa, watahiniwa 528,336 sawa na asilimia 47.7 walichagua jibu sahihi A, *kuamua*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu nahau kata shauri yenye maana ya kuamua hivyo kuchagua jibu lenye maana ya nahau husika.

Hata hivyo, watahiniwa 564,271 sawa na asilimia 50.9 walichagua kati ya vipotoshi B *kuwatahadharisha*, C *kuwaasa*, D *kuonya* na E *kufundisha*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *kuwatahadharisha*

walishindwa kuelewa kuwa maana yake ni kuepukana na jambo. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *kuwaasa* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo humaanisha kumwambia mtu asifanye jambo fulani. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *kuonya* walishindwa kuelewa kuwa maana yake ni kutoa tahadhari. Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *kufundisha* walishindwa kuelewa kuwa maana yake ni kutoa mafunzo au kuelimisha. Hivyo uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha juu ya nahau mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.

Swali la 13: Chekacheka anapenda watoto wake wawe na tabia njema hadi ukubwani. Methali ipi kati ya zifuatazo inahimiza tabia ya aina hiyo?

A Zimwi likujualo halikuli likakwisha.
B Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
C Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
D Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.
E Tabia hupamba kuliko libasi.

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kueleza mafunzo anayoyapata katika methali na kuhusianisha na maisha ya kila siku. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 10 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 10: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	49,928	71,281	823,348	63,136	88,276	11,806
Asilimia ya Watahiniwa	4.5	6.4	74.3	5.7	8.0	1.1

Jedwali Na. 10 linaonesha kuwa, watahiniwa 823,348 sawa na asilimia 74.3 walichagua jibu sahihi C *Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha juu ya mafunzo yanayopatikana katika methali husika.

Hata hivyo, watahiniwa 272,616 sawa na asilimia 24.6 walichagua kati ya vipotoshi A *zimwi likujualo halikuli likakwisha*, B *asiyesikia la mkuu huvunjika guu*, D *umoja ni nguvu utengano ni dhaifu* na E *tabia hupamba kuliko libasi*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *zimwi likujualo halikuli likakwisha* walishindwa kuelewa kuwa methali hii inafundisha kuwa, mtu wako wa karibu hawezi kukufanyia uovu. Waliochagua kipotoshi *asiyesikia la mkuu huvunjika guu*, hawakuelewa kuwa methali hii hushauri watu umuhimu wa kufuata ushauri wa wazazi au watu waliokuzidi maarifa.

Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *umoja ni nguvu utengano ni udhaifu* hawakuelewa kuwa methali hiyo inatufundisha tuwe na ushirikiano katika mambo mbalimbali. Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi, *tabia hupamba kuliko libasi*, hawakufahamu kuwa methali hii inatufunza kuwa, tabia nzuri huvutia watu zaidi kuliko mavazi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki walifananisha mafunzo ya swali husika na methali *tabia hupamba kuliko libasi* kutokana na matumizi ya neno tabia lilivyojitokeza. Kwa ujumla watahiniwa hao hawakuwa na

umahiri wa kutosha wa kueleza mafunzo yanayopatikana katika methali kulingana na maisha ya kila siku.

Swali la 14: “Nikitembea walio wafu huamka na walio hai hukaa kimya.”

Jibu la kitendawili hiki ni lipi kati ya yafuatayo?

A Nyuki ndani na nje ya mzinga

B Yai na kifaranga chake

C Majani makavu na mabichi

D Kulala usingizi na kuamka

E Tumbo na chakula

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa watahiniwa katika kutega na kutegua vitendawili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 11 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 11: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	151,279	124,420	587,166	129,666	100,998	14,246
Asilimia ya Watahiniwa	13.7	11.2	53.0	11.7	9.1	1.3

Jedwali Na. 11 linaonesha kuwa, watahiniwa 587,166 sawa na asilimia 53.0 walichagua jibu sahihi C *majani makavu na mabichi.* Watahiniwa hao waliweza kuelewa kuwa majani makavu yakikanyagwa hutoa sauti ambayo hufananishwa na kifungu cha maneno *wafu huamka* na majani mabichi yakikanyagwa hayatoi sauti ambayo hufananishwa na kifungu cha maneno *walio hai hukaa kimya*. Huu ni uthibitisho kuwa watahiniwa

hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya fumbo lililojengwa katika kitendawili husika.

Watahiniwa 506,358 sawa na asilimia 32.1 walichagua kati ya vipotoshi A *nyuki ndani na nje ya mzinga* B *yai na* kifaranga *chake* D *kulala usingizi na kuamka* na E *tumbo na chakula.* Watahiniwa waliochagua *nyuki ndani na nje ya mzinga* hawakuweza kubaini kuwa hili ni jibu la kitendawili *watoto wa mfalme wale wanaingia na wale wanatoka* ambalo halihusiani kabisa na kitendawili husika. Pia, watahiniwa waliochagua *yai na kifaranga chake,* hili ni jibu la kitendawili *mzazi ana miguu mzaliwa hanayo*. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *kulala usingizi na kuamka* ni jibu la kitendawili *kila siku ninakufa na kufufuka tena*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *tumbo* na *chakula* walihusianisha tumbo na walio wafu na chakula walio hai ambapo vifungu hivyo vya maneno vipo katika kitendawili husika.

Swali la 15: Ni methali ipi kati ya zifuatazo ina maana sawa na methali "akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki?"

A Baniani mbaya kiatu chake dawa.

B Damu nzito kuliko maji.

C Undugu kufaana si kufanana.

D Shukrani ya punda mateke.

E Sikio la kufa halisikii dawa.

Swali lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua methali zenye maana sawa katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 12

linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 12: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	197,597	249,161	476,375	74,408	99,334	10,900
Asilimia ya Watahiniwa	17.8	22.5	43.0	6.7	9.0	1.0

Jedwali Na. 12 linaonesha kuwa watahiniwa 476,375 sawa na asilimia 43.0 walichagua jibu sahihi C *undugu kufaana si kufanana.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha juu ya maana ya methali husika kuwa mtu anayekufaa au kukusaidia wakati wa shida ndiye rafiki hivyo kuweza kufananisha na methali "akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki".

Aidha, watahiniwa 257,000 sawa na asilimia 56.0 walichagua kati ya vipotoshi A *baniani mbaya kiatu chake dawa*, B *damu nzito kuliko maji*, D *shukrani ya punda mateke* na E *sikio la kufa halisikii dawa*. Uteuzi wa kipotoshi *baniani mbaya kiatu chake dawa* haukuwa sahihi kwani watahiniwa walishindwa kuelewa maana ya methali hiyo kuwa mtu hawezi kuwa na ubaya tu, kuna wakati ana uzuri wake. Pia, waliochagua kipotoshi *damu nzito kuliko maji* walishindwa kuelewa kuwa, methali hiyo inamaanisha kuwa uhusiano wa kidamu ni muhimu sana hivyo walielewa kuwa anayeweza kukusaidia ni ndugu na si mtu mwingine. Watahiniwa wengine waliochagua kipotoshi *shukrani ya punda ni mateke* walishindwa kuelewa kuwa unaweza kufanya wema lakini ukalipwa ubaya. Watahiniwa waliochagua *sikio la kufa halisikii dawa* walishindwa kuelewa kuwa methali hii ina maana kuwa jambo ambalo limeandikwa kuharibika halinabudi kuharibika hata kama juhudi nyingi sana ya kusaidia zitafanyika. Kwa ujumla watahiniwa hao walishindwa kubaini

kuwa maana ya methali hizo hazina uhusiano kabisa na methali *akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki* yenye maana, mtu anayekusaidia wakati wa shida ndiye rafiki wa kweli.

Swali la 16: Neno lipi kati ya yafuatayo ni jumuishi kwa maneno haya "nyanya, vitunguu, pilipili na tangawizi?"

A Nafaka

B Matunda

C Vinywaji

D Vitoweo

E Viungo

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 13 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 13: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C	D	E*	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	34,563	37,739	30,683	34,888	961,584	8,318
Asilimia ya Watahiniwa	3.1	3.4	2.8	3.1	86.8	0.8

Jedwali Na. 13 linaonesha kuwa, watahiniwa 961,584 sawa na asilimia 86.8 walichagua jibu sahihi E *viungo*. Watahiniwa hao waliweza kuelewa kuwa *nyanya, vitunguu, pilipili* na *tangawizi* ni viungo vinavyotumika kuongeza ladha katika mapishi ya vyakula mbalimbali. watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya maana ya msamiati *viungo*.

Hata hivyo, watahiniwa 137,873 sawa na asilimia 12.4 walishindwa kubaini neno jumuishi la *nyanya, vitunguu, pilipili na tangawizi* kwa kuandika vipotoshi A *nafaka,* B *matunda*, C *vinywaji*, D *vitoweo.* Watahiniwa walioandika *nafaka* walishindwa kubaini kuwa nafaka ni punje za mimea kama vile mtama, mahindi, mpunga na uwele zinazotumiwa kama chakula. Pia, waliochagua *matunda* walishindwa kuelewa kuwa matunda ni zao la mmea linalohifadhi mbegu ambalo hutokana na ua. Aidha, waliochagua kipotoshi *vinywaji,* walishindwa kuelewa kuwa kinywaji ni kitu cha majimaji kinachonywewa kama vile uji, chai, maziwa, soda na togwa. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *vitoweo,* hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa kuwa kitoweo ni kitu kama vile mchuzi, mboga, samaki au nyama kinachotumiwa kwa kulia chakula.

Swali 17: Mwaka 1985 Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliamua kung'atuka madarakani na kumwachia Mheshimiwa, Ali Hassan Mwinyi. Kitendo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kung'atuka kinamaanisha nini?

A Kuaga wafanyakazi

B Kuwaachia wafanyakazi

C Kustaafu kazi

D Kujiuzulu madaraka

E Kupumzika kazi kidogo

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali

hili kilikuwa hafifu. Jedwali Na. 14 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 14: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C	D*	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	40,564	32,981	592,286	393,263	37,959	10,722
Asilimia ya Watahiniwa	3.7	3.0	53.5	35.5	3.4	1.0

Jedwali Na. 14 linaonesha kuwa watahiniwa 703,790 sawa na asilimia 63.50 walichagua kati ya vipotoshi A *kuaga wafanyakazi*, B *kuwaachia wafanyakazi*, C *kustaafu kazi* na E *kupumzika kazi kidogo*. Waliochagua kipotoshi *kuaga wafanyakazi*, hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa maana sahihi ya msamiati *kuaga* kuwa ni kuomba ruhusa ya kuondoka. Waliochagua kipotoshi *kuwaachia wafanyakazi* walishindwa kuelewa kuwa kuachia lina maana ya kutengana na mtu, kitu, jambo au hali. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *kustaafu kazi* walishindwa kuelewa kuwa kustaafu maana yake ni kuacha kazi ya kuajiriwa baada ya kufikia muda au umri maalumu uliowekwa. Aidha, walichagua kipotoshi *kupumzika kazi kidogo* walishindwa kuelewa kuwa kupumzika ina maana kuwa kupata muda wa kutuliza mwili baada ya kazi fulani.

Hata hivyo, watahiniwa 393,263 sawa na asilimia 35.50 walichagua jibu sahihi D *kujiuzulu madarakani* likiwa na maana ya kuacha kazi kwa hiari. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha ya kuweza kuelewa maana sahihi ya msamiati ng’atuka kuwa na maana sawa na neno kujiuzulu.

Swali la 18: Neno lipi kati ya yafuatayo ni jumuishi kwa maneno haya "almasi, dhahabu, tanzanaiti na lulu?"

A Shaba

B Vyuma

C Marumaru

D Mgodi

E Madini

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Kielelezo Na. 4 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Kielelezo Na. 4: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.*

Kielelezo Na. 4 kinaonesha kuwa, watahiniwa 946,800 sawa na asilimia 85.50 waliochagua jibu sahihi E, *madini* walikuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa kuwa madini ni kitu kinachochimbwa ardhini kama vile, chuma, shaba, bati, fedha, dhahabu, almasi, mafuta na tanzanaiti. Hivyo waliweza kubaini neno moja linalojumuisha maneno hayo kuwa ni madini.

Hata hivyo, watahiniwa 151,021 sawa na asilimia 13.6 walichagua kati ya vipotoshi A *shaba* B *vyuma*, C *marumaru* na D, *mgodi*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi *shaba* na *vyuma* walishindwa kuelewa kuwa haya ni aina ya madini yanayochimbwa ardhini na siyo neno jumuishi la kuwakilisha madini yote. Pia, waliochagua kipotoshi *marumaru* walishindwa kuelewa kuwa ni jiwe linalong'aa vizuri ambalo hutumika kama pambo la kuta za nyumba na wasifu. Aidha, waliochagua *mgodi,* walishindwa kuelewa kuwa neno mgodi lina maana ya mahali panapochimbuliwa madini kama vile, dhahabu, makaa ya mawe au almasi. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walishindwa kuelewa maana ya msamiati madini.

Swali la 19: Katika neno "ninakula" kiambishi cha wakati uliopo ni kipi kati ya vifuatavyo?

A -ni-

B -ku-

C -na-

D -la-

E -kul-

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa

mtahiniwa kuelewa nyakati mbalimbali katika sentensi za lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 15 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 15: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	202,624	80,412	670,814	38,146	104,651	11,128
Asilimia ya Watahiniwa	18.3	7.3	60.6	3.4	9.4	1.0

Jedwali Na. 15 linaonesha kuwa watahiniwa 670,814 sawa na asilimia 60.60 walichagua jibu sahihi C –na- walikuwa na umahiri wa kutosha wa kubaini kiambishi cha wakati uliopo ambacho ni –na-, katika kitenzi *ninakula*.

Watahiniwa 425,833 sawa na asilimia 38.4 walichagua kati ya vipotoshi A –ni-, B, –ku-, D, –la-, na E, –kul-. Watahiniwa waliochagua kipotoshi –ni- walishindwa kuelewa kuwa kiambishi –ni- kinawakilisha nafsi ya kwanza umoja na si kiambishi cha wakati uliopo. Vilevile, waliochagua kipotoshi –ku- walishindwa kuelewa kuwa kiambishi hicho hurejelea mtenda wa jambo ambaye ni yule mlaji katika kitenzi husika. Waliochagua kipotoshi –la- walishindwa kuelewa kuwa ni moja wapo ya silabi inayounda neno husika. Pia watahiniwa waliochagua kipotoshi –kul- walishindwa kuelewa kuwa viambishi hivyo ni fonimu zinazounda neno husika. Kwa ujumla uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kiambishi cha wakati uliopo ambacho ni -na- katika neno *ninakula*.

Swali la 20: “Muda ulipowadia wanafunzi wote tulisimama foleni”. Neno “wadia” linashabihiana na neno lipi kati ya yafuatayo?

A fika

B kwisha

C patikana

D pungua

E ongezeka

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Kielelezo Na. 5 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Kielelezo Na. 5*: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.*

Kielelezo Na. 5 kinaonesha kuwa watahiniwa 899,636 sawa na asilimia 81.2 walichagua jibu sahihi A *fika*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri

wa kutosha wa kuelewa maana ya neno *wadia* kuwa ni kufika au kutimia kwa wakati.

Hata hivyo, watahiniwa 198,959 sawa na asilimia 18.0 walichagua kati ya vipotoshi B *kwisha*, C *patikana*, D *pungua* na E *ongezeka*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *kwisha* walishindwa kuelewa maana ya msamiati huo kuwa ni kufika mwisho wa kitu au jambo. Watahiniwa waliochagua kipotoshi patikana walishindwa kuelewa kuwa neno hilo humaanisha kuweza kuonekana sehemu mbalimbali. Aidha, waliochagua kipotoshi *pungua* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo linamaanisha kuwa ndogo zaidi ya kiwango kilichotakiwa. Pia, waliochagua kipotoshi *ongezeka*, walishindwa kuelewa kuwa neno hilo humaanisha kitu kilichozidi au ziada. Hivyo watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wakutosha kuelewa maana ya misamiati mbalimbali hususani katika neno “wadia” kuwa ni fika au timia wakati.

Swali la 21: Katika sentensi “Wimbo wa Taifa umeimbwa kwa ustadi.” Neno lipi kati ya yafuatayo limesimama kama kitenzi?

A wimbo
B ustadi
C taifa
D kwa
E umeimbwa

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kubaini aina za maneno katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani.

Jedwali Na: 16 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 16: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C	D	E*	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	122,661	153,207	129,018	130,077	559,958	12,854
Asilimia ya Watahiniwa	11.1	13.8	11.6	11.7	50.5	1.2

Jedwali Na. 16 linaonesha kuwa watahiniwa 559,958 sawa na asilimia 50.55 walichagua jibu sahihi E *umeimbwa*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa kuwa kitenzi ni neno linalotaja tendo lilivyotendeka au litakavyotendeka katika sentensi, hivyo kuweza kubaini kitenzi *umeimbwa* katika sentensi husika.

Watahiniwa 534,963 sawa na asilimia 48.29 walichagua kati ya vipotoshi A *wimbo*, B *ustadi,* C *taifa*, D *kwa.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi A *wimbo*, hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa kuwa neno wimbo limetumika kama nomino katika sentensi husika. Watahiniwa waliochagua kipotoshi B *ustadi,* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo limetumika kama kielezi katika sentensi husika. Aidha, waliochagua kipotoshi C *taifa* hawakuwa na umahiri wa kuelewa kuwa neno taifa si kitenzi bali ni nomino katika sentensi husika. Pia, waliochagua kipotoshi D *kwa,* hawakuwa na umahiri wa kutosha kuelewa kuwa neno *kwa* limetumika kama kihusishi na sio kitenzi kama swali lilivyotaka. Kwa ujumla uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa aina za maneno hasa kitenzi katika sentensi.

Swali la 22: Neno lipi halilandani na mengine kati ya maneno yafuatayo?

A Kuku

B Bata

C Kaa

D Mwewe

E Kunguru

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Kielelezo Na: 6 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo



Kielelezo Na. 6: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.*

Kielelezo Na: 6 kinaonesha kuwa, watahiniwa 978,893 sawa na asilimia 88.4 walichagua jibu sahihi C *kaa.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri

wa kutosha wa kuelewa kuwa kuku, bata, mwewe na kunguru wote hawa ni ndege ambao ni viumbe wenye mabawa na manyoya ambao huruka angani. Lakini kaa ni mnyama mdogo wa majini mwenye miguu sita au zaidi mwenye gamba mwilini.

Watahiniwa 119,114 sawa na asilimia 10.7 walichagua kati ya vipotoshi A *kuku*, B *bata*, D *mwewe* na E *kunguru*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walishindwa kuelewa kuwa hao ni ndege ambao ni viumbe wenye mabawa na manyoya ambao huruka angani. Hivyo, wote wana sifa zinazofanana.

Swali la 23: "Mtoto mzuri anajua kupangilia ratiba." Katika sentensi hii, neno lipi kati ya yafuatayo limetumika kama kivumishi.

A mzuri
B mtoto
C kupangilia
D ratiba
E anajua

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia msamiati katika mazungumzo kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuelewa aina za maneno katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na: 17 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 17: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	738,961	116,102	94,769	50,412	96,333	11,198
Asilimia ya Watahiniwa	66.7	10.5	8.6	4.6	8.7	1.0

Jedwali Na. 17 linaonesha kuwa, watahiniwa 738,961 sawa na asilimia 66.7 walichagua jibu sahihi A *mzuri*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kufahamu aina za maneno hivyo waliweza kujua kuwa kivumishi ni neno linalotoa taarifa kuhusu nomino au kiwakilishi katika sentensi. hivyo waliweza kubaini kuwa neno *mzuri* ni kivumishi cha sifa.

Hata hivyo, watahiniwa 357,616 sawa na asilimia 32.3 walichagua kati ya kipotoshi B *mtoto*, C *kupangilia*, D *ratiba*, na E *anajua*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *mtoto* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo ni nomino kwa kuwa hutaja mtenda wa jambo na wala si kivumishi katika sentensi husika. Waliochagua kipotoshi *kupangilia* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo ni kitenzi kikuu ambacho hutoa taarifa ya mtenda katika sentensi husika. Waliochagua kipotoshi *ratiba* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo ni nomino inayotokea upande wa kiarifu katika sentensi husika. Aidha, waliochagua kipotoshi *anajua* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo ni kitenzi kisaidizi ambacho huhitaji kitenzi kikuu kukamilisha maana. Kwa ujumla watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kufahamu aina za maneno katika sentensi.

Swali la 24: “Hawa ndio wapole darasani mwetu.” Katika sentensi hii, neno lipi kati ya yafuatayo limetumika kama kiwakilishi?

A ndio
B hawa
C wapole
D darasani
E mwetu

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia msamiati katika mazungumzo kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuelewa aina za maneno katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na: 18 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 18: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	120,193	638,768	211,637	79,816	45,808	11,553
Asilimia ya Watahiniwa	10.8	57.7	19.1	7.2	4.1	1.0

Jedwali Na: 18 linaonesha kuwa watahiniwa 638,768 sawa na asilimia 57.7 walichagua jibu sahihi B *hawa*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu aina za maneno hivyo waliweza kubaini kuwa neno “hawa” ni kiwakilishi kioneshi ambacho huwakilisha nomino ambayo hutaja majina ya watu.

Aidha, watahiniwa 457,454 sawa na asilimia 41.3 waliochagua kati ya vipotoshi A *ndio*, C *wapole*, D *darasani* na E *mwetu*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndio* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo ni kitenzi kishirikishi ambacho hukamilisha maana katika sentensi. Waliochagua kipotoshi *wapole* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo ni kivumishi ambacho hutoa sifa ya ziada kwa nomino iliyowakilishwa na kiwakilishi *hawa* katika sentensi husika. Aidha, waliochagua kipotoshi darasani walishindwa kuelewa kuwa neno hilo ni kielezi cha mahali ambacho hueleza namna au jinsi tendo lilivyotendeka. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *mwetu* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo si

kiwakilishi bali ni kielezi kama lilivyotumika katika sentensi husika. Kwa ujumla watahiniwa hao walikosa umahiri wa kutosha kuhusu aina za maneno.

Swali la 25: Ni neno lipi kati ya yafuatayo linakamilisha sentensi hii kwa usahihi? “Nikisoma kwa bidii _____ mtihani wangu.”

A ningefaulu

B nitafaulu

C ningalifaulu

D ningelifaulu

E ninafaulu

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia msamiati katika mazungumzo kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika upatanisho wa kisarufi hasa kwa kuangalia hali ya umoja na wingi katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 19 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 19: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	63,685	873,616	58,846	55,083	46,673	9,872
Asilimia ya Watahiniwa	5.7	78.9	5.3	5.0	4.2	0.9

Jedwali Na. 19 linaonesha kuwa, watahiniwa 873,616 sawa na asilimia 78.9 walichagua jibu sahihi B *nitafaulu*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kubaini upatanisho wa kisarufi katika sentensi zenye muundo wa masharti katika sentensi shurutia. Hivyo waliweza kutambua kuwa, upande mmoja wa swali ukiwa na kiambishi cha

masharti –**ki**- upande wa pili wa swali lazima uundwe na kiambishi –**ta**- kukamilisha upatanisho wa kisarufi.

Watahiniwa 224,287 sawa na asilimia 20.2 walichagua kati ya vipotoshi A *ningefaulu*, C *ningalifaulu*, D *ningelifaulu*, E *ninafaulu.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ningefaulu* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hicho hakina upatanisho wa kisarufi na swali husika kwa kuwa kiambishi –ki- katika neno *nikisoma* hakina upatanisho na kiambishi –nge- katika neno *ningefaulu*. Waliochagua kipotoshi *ningalifaulu* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hicho hakina upatanisho wa kisarufi na swali husika kwa kuwa kiambishi –ki- katika neno *nikisoma* hakina upatanisho na kiambishi –ngali- katika neno *ningalifaulu.* Aidha, uteuzi wa kipotoshi *ningelifaulu* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hicho hakina upatanisho wa kisarufi na swali husika kwa kuwa kiambishi –ki- katika neno *nikisoma* hakina upatanisho na kiambishi –ngeli- katika neno *ningelifaulu*. Vilevile, waliochagua kipotoshi *ninafaulu* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hiki hakina upatanisho wa kisarufi na swali husika kwa kuwa kiambishi –ki- katika neno *nikisoma* hakina upatanisho na kiambishi –na- katika neno *ninafaulu.* Kwa ujumla watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu upatanisho wa kisarufi katika sentensi.

Swali la 26: “Nitakula uji wangu kesho asubuhi.” Sentensi hii imekosewa. Sentensi sahihi ni ipi kati ya zifuatazo?

A Nitamung’unya uji wangu kesho asubuhi.

B Nitatafuna uji wangu kesho asubuhi.

C Nitakunywa uji wangu kesho asubuhi.

D Nitameza uji wangu kesho asubuhi.

E Nitabugia uji wangu kesho asubuhi.

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia msamiati katika mazungumzo kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuunda sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri sana. Kielelezo Na. 7 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Kielelezo.Na 7: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.*

Kielelezo Na. 7 kinaonesha kuwa, watahiniwa 982,490 sawa na asilimia 88.7 walichagua jibu sahihi C *nitakunywa uji wangu kesho asubuhi*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kupangilia maneno na kuunda sentensi. Aidha, waliweza kuelewa kuwa sentensi hiyo huundwa na T + N + V + E.

Hata hivyo, watahiniwa 115,905 sawa na asilimia 10.5 walichagua kati ya vipotoshi A *nitamung'unya uji wangu kesho asubuhi*, B *nitatafuna uji wangu kesho asubuhi*, D *nitameza uji wangu kesho asubuhi* na E *nitabugia uji wangu kesho asubuhi*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walikuwa hawana umahiri wa kutosha wa kuunda sentensi. Hivyo

kushindwa kuelewa kuwa mpangilio wa maneno hayo yaliyounda hizo tungo yalikuwa hayana upatanisho wa kisarufi hivyo hakuna uhusiano kati ya neno moja na maneno mengine yanayounda tungo hizo.

Swali la 27: "Kijiji chetu kina maendeleo duni lakini mwaka ujao itakuwa kinyume chake." Je, mwaka ujao kijiji chetu kitakuwa na maendeleo gani?

A Imara

B Dhaifu

C Mabaya

D Hafifu

E Dhahiri

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 20 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 20: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	810,816	91,522	73,036	55,966	67,365	9,070
Asilimia ya Watahiniwa	73.2	8.3	6.6	5.1	6.1	0.8

Jedwali Na. 20 linaonesha kuwa watahiniwa 810,816 sawa na asilimia 73.2 waliweza kuchagua jibu sahihi A *imara*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha juu ya maana ya misamiati mbalimbali na kinyume chake. Hivyo waliweza kubaini kuwa neno *duni* lina maana ya

hafifu. Watahiniwa hao waliweza kubaini kinyume cha neno duni kuwa ni *imara* ambalo lina maana ya hali ya kuwa madhubuti.

Hata hivyo, watahiniwa 287,889 sawa na asilimia 26.0 walichagua kati ya vipotoshi B *dhaifu*, C *mabaya*, D *hafifu* na E *dhahiri.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *dhaifu* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina maana ya unyonge au kudhoofu. Waliochagua kipotoshi *mabaya* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina maana ya hitilafu. Aidha, waliochagua kipotoshi *hafifu* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina maana ya kuwa na thamani ndogo, isiyofaa, duni au hafifu. Vilevile, uteuzi wa kipotoshi *dhahiri* haukuwa sahihi kwa kuwa neno dhahiri lina maana ya bila kuficha, bayana au waziwazi. Kwa ujumla watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu maana ya msamiati na kinyume chake katika swali husika.

Swali la 28: Maneno yapi kati ya yafuatayo yapo katika mpangilio sahihi kwa kuzingatia matumizi ya kamusi?

A fana, fani, faraja, farasi
B fana, faraja, farasi, fani
C fana, farasi, faraja, fani
D fani, fana, faraja, farasi
E fana, farasi, fani, faraja

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kutumia kamusi ili kueleza maana za maneno yaliyotumika katika habari. Kiwango cha ufaulu katika

swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 21 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 21 Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	488,676	202,893	126,982	194,245	82,313	12,666
Asilimia ya Watahiniwa	44.1	18.3	11.5	17.5	7.4	1.1

Jedwali Na. 21 linaonesha kuwa, watahiniwa 488,676 sawa na asilimia 44.1 walichagua jibu sahihi A *fana, fani, faraja, farasi*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kubaini mpangilio sahihi wa herufi za alfabeti za Kiswahili kwa kutumia kamusi.

Hata hivyo, watahiniwa 606,433 sawa na asilimia 54.7 waliochagua kati ya vipotoshi B *fana, faraja, farasi, fani* C *fana, farasi, faraja, fani* D *fani fana faraja, farasi* na E *fana, farasi, fani, faraja*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi *hivyo* hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kubaini mpangilio wa herufi za alfabeti za maneno ya Kiswahili kwa kutumia kamusi. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa maneno *fana, fani, faraja, farasi* yamepangwa kwa kufuata mpangilio wa alfabeti.

Swali la 29: Kitenzi kipi kati ya vifuatavyo kinatokana na nomino "mchemsho?"

A Mchemshaji

B Chemsha

C Chemshika

D Chemshana

E Chemshiana

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kutumia nomino kuunda kitenzi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 22 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 22: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	270,545	659,055	81,436	43,133	42,845	10,761
Asilimia ya Watahiniwa	24.4	59.5	7.4	3.9	3.9	1.0

Jedwali Na. 22 linaonesha kuwa watahiniwa 659,055 sawa na asilimia 59.5 walichagua jibu sahihi B *chemsha*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kubaini kuwa kitenzi *chemsha* hutokana na nomino “mchemsho.”

Hata hivyo, watahiniwa 437,959 sawa na asilimia 39.5 walichagua kati ya vipotoshi A *mchemshaji*, C *chemshika*, D *chemshana* na E *chemshiana*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *mchemshaji* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo ni nomino na wala si kitenzi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *chemshika* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lipo katika kauli ya kutendeka na huwa na kiambishi –ik-. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *chemshana* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lipo katika kauli ya kutendana na huwa na kiambishi –an- Aidha, waliochagua kipotoshi *chemshiana* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lipo katika kauli ya kutendeana na huwa na kiambishi -ian-. Kwa ujumla watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kuunda kitenzi kutokana na nomino husika.

Swali la 30: Ni nomino ipi inaundwa kutokana na neno “chunga?”

A Chungana

B Chungiana

C Mchungaji

D Chungika

E Chungisha

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kutumia kitenzi kuunda nomino. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 23 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 23: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	121,474	69,187	794,757	61,652	49,698	11,007
Asilimia ya Watahiniwa	11.0	6.2	71.7	5.6	4.5	1.0

Jedwali Na. 23 linaonesha kuwa, watahiniwa 794,754 sawa na asilimia 71.7 walichagua jibu sahihi C *mchungaji*. Watahiniwa walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu unominishaji wa kitenzi “chunga”. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa neno mchungaji ni nomino ila maneno chungana, chungiana, chungika na chungisha ni vitenzi vilivyopo katika kauli za utendaji.

Hata hivyo, watahiniwa 302,011 sawa na asilimia 27.3 walichagua kati ya vipotoshi A *chungana*, B *chungiana*, D *chungika* na E *chungisha*. Watahiniwa waliochagua *chungana* hawakuwa na uelewa kuwa

kipotoshi hiki kipo katika kauli ya kutendana. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *chungiana* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hiki kipo katika kauli ya kutendeana. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *chungika* hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kubaini kuwa neno hilo lipo katika kauli ya kutendeka. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *chungisha* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hicho kipo katika kauli ya kutendesha. Kwa jumla watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kuunda nomino kutokana na kitenzi *chunga*.

Swali la 31: "Polepole ndio mwendo." Methali hii inahusiana na methali ipi kati ya hizi zifuatazo?

A Maneno mengi hula matendo.

B Chembe na chembe mkate huwa.

C Chanda chema huvikwa pete.

D Shukrani ya punda ni mateke.

E Dua la kuku halimpati mwewe.

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kueleza maana inayopatikana katika methali mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu. Jedwali Na. 24 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 24: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	180,972	440,892	234,646	107,855	129,210	14,200
Asilimia ya Watahiniwa	16.3	39.8	21.2	9.7	11.7	1.3

Jedwali Na. 24 linaonesha kuwa, watahiniwa 652,683 sawa na asilimia 58.4 walichagua kati ya vipotoshi A *maneno mengi hula matendo*, C *chanda chema huvikwa pete*, D *shukrani ya punda mateke* na E *dua la kuku halimpati mwewe*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *maneno mengi hula matendo* walishindwa kuelewa kuwa methali hii ina maana kuwa ukiwa mzungumzaji sana huwezi kufanya kazi kwa ufanisi, muda mwingi utapotelea kwenye mazungumzo. Hivyo, methali hii haina uhusiano na methali husika katika swali. Waliochagua kipotoshi *chanda chema huvikwa pete* walishindwa kuelewa kuwa methali hii hutumika kuelezea kuwa tuzo hupewa mtu mwenye sifa nzuri. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *shukrani ya punda ni mateke hawakuwa na uelewa wa maana ya* methali inayomaanisha kuwa unaweza kufanya wema lakini ukalipwa ubaya. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *dua la kuku halimpati mwewe* methali yenye maana kuwa maapizo ya mtu mnyonge dhidi ya mtu mwenye mamlaka hayawezi kumdhuru asilani, hawakuelewa maana yake. Kwa ujumla watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa maana ya methali mbalimbali na kuhusianisha na methali tajwa katika swali husika.

Hata hivyo, watahiniwa 440,892 sawa na asilimia 30.8 walichagua jibu sahihi B *chembe na chembe mkate huwa*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa maana ya methali *polepole ndio mwendo* ikiwa na maana kuwa tufanye mambo yetu kwa utaratibu ikiwa tunataka yafanikiwe au yafane. Hivyo, watahiniwa waliweza kubaini kuwa methali *chembe na chembe mkate huwa* inahusiana na methali husika ikiwa na maana kuwa ukiweka kitu kidogo kidogo huishia kupata kitu kikubwa.

Swali la 32: Charubuma alionywa na wazazi wake kuacha tabia ya wizi, lakini hakuwasikiliza hatimaye alifungwa jela. Methali gani kati ya zifuatazo inakemea tabia hiyo isiyofaa katika jamii?

A Asiye na mwana aeleke jiwe.

B Asiye na lake hafungi safari mapema.

C Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

D Asiye na bahati habahatishi.

E Asiye na mengi ana machache.

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kueleza mafunzo yanayopatikana katika methali mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 25 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 25: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	35,772	44,519	962,158	30,209	25,655	9,462
Asilimia ya Watahiniwa	3.2	4.0	86.9	2.7	2.3	0.9

Jedwali Na. 25 linaonesha kuwa watahiniwa 962,158 sawa na asilimia 86.9 walichagua jibu sahihi C *asiyesikia la mkuu huvunjika guu*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa funzo linalopatikana katika methali husika kuwa ni muhimu kuwasikiliza wakubwa au watu wanaotuzidi maarifa wakiwa wanatuonya kuhusu kuacha tabia mbaya.

Hata hivyo, watahiniwa 136,155 sawa na nasilimia 12.2 walichagua kati ya vipotoshi A *asiye na mwana aeleke jiwe*, B *asiye na lake hafungi*

safari mapema, D *asiye na bahati habahatishi* na E *asiye na mengi ana machache*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *asiye na mwana aeleke jiwe* walishindwa kuelewa kuwa methali hiyo inatufunza umuhimu wa kujiandaa kutafuta kitu ukitakacho usingoje kuletewa au kujileta chenyewe. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *asiye na lake hafungi safari mapema* walishindwa kuelewa kuwa methali hii inatoa mafunzo kuhusu umuhimu wa kujitegemea badala ya kutegemea wengine.

Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *asiye na bahati habahatishi*, walishindwa kuelewa kuwa methali hii inatufunza umuhimu wa mtu kutenda jambo fulani vizuri bila kuhitaji kitu chochote kama malipo maana hata ukifanya kitu kizuri hakuna atakayejali au atakayethamini kitu hicho. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *asiye na mengi ana machache* walishindwa kuelewa kuwa methali hii inatufundisha kuwa, hakuna binadamu asiye na changamoto au mafanikio awe tajiri au maskini. Kwa ujumla watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kujua mafunzo yanayopatikana katika methali, hivyo kushindwa kubainisha methali inayokemea tabia husika.

Swali la 33: Hakuna msiba _____". Kifungu kipi cha maneno kati ya vifuatavyo kinakamilisha methali hii?

A usiokuwa na vilio
B usiokuwa na mwenziwe
C usiokuwa na chakula
D usiokuwa na matanga
E usiokuwa na watu

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa

katika kutambua muundo wa methali za Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 26 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 26: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B*	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	229,300	538,300	44,445	153,935	129,877	11,918
Asilimia ya Watahiniwa	20.7	48.6	4.0	13.9	11.7	1.1

Jedwali Na. 26 linaonesha kuwa, watahiniwa 538,300 sawa na asilimia 48.6 walichagua jibu sahihi B *usiokuwa na mwenziwe.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu muundo sahihi wa methali huwa na pande mbili zinazotegemeana kidhima na kimaana.

Hata hivyo, watahiniwa 557,557 sawa na asilimia 50.3 walichagua kati ya vipotoshi A *usiokuwa na vilio*, C *usiokuwa na chakula*, D *usiokuwa na matanga* na E *usiokuwa na watu*. Watahiniwa walichagua kipotoshi *usiokuwa na vilio* walihusisha msiba na vilio vya waombelezaji. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *usiokuwa na chakula* walihusisha msiba na chakula kinachotolewa msibani. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *usiokuwa na matanga* walihusisha msiba na maombolezo msibani. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *usiokuwa na watu* walihusisha msiba na watu wanaofika msibani kuombeleza. Kwa ujumla watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu muundo wa methali hivyo kushindwa kukamilisha methali husika.

Swali la 34: Kirefu cha neno BAKITA ni kipi kati ya maneno yafuatayo?

A Baraza la Sanaa la Taifa

B Baraza la Mitihani la Tanzania

C Baraza la Michezo Tanzania

D Baraza la Kiswahili la Taifa

E Baraza la Kiswahili la Zanzibar

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia maandishi katika kuwasiliana kulingana na miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuandika kirefu cha vifupisho vya maneno. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 27 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 27: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C	D*	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	90,456	108,725	59,920	805,006	32,354	11,314
Asilimia ya Watahiniwa	8.2	9.8	5.4	72.7	2.9	1.0

Jedwali Na. 27 linaonesha kuwa watahiniwa 805,006 sawa na asilimia 72.7 walichagua jibu sahihi D *Baraza la Kiswahili la Taifa*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kirefu cha neno *BAKITA* kuwa ni *Baraza la Kiswahili la Taifa*" ambapo *BA* ni kifupisho cha neno Baraza, *KI* ni kifupisho cha neno Kiswahili na *TA* ni kifupisho cha neno Taifa.

Hata hivyo, watahiniwa 291,455 sawa na asilimia 26.3 walichagua kati ya vipotoshi A *Baraza la Sanaa la Taifa*, B *Baraza la Mitihani la Tanzania*, C *Baraza la Michezo Tanzania*, E *Baraza la Kiswahili Zanzibar*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *Baraza la Sanaa la Taifa*

hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa kuwa *Baraza la Sanaa la Taifa* ni kirefu cha neno *BASATA*. Waliochagua kipotoshi *Baraza la Mitihani la Tanzania* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hicho ni kirefu cha neno *BMT*. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *Baraza la Michezo Tanzania* walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hicho ni kirefu cha neno *BMT*. Aidha, waliochagua kipotoshi *Baraza la Kiswahili la Zanzibar* ni kirefu cha neno *BAKIZA*.

Swali la 35: Katika uandishi wa kumbukumbu za mkutano saini ya mwenyekiti hukaa sehemu gani?

A Mwanzoni mwa kichwa cha kumbukumbu

B Katikati ya kumbukumbu kwenye ajenda za mkutano

C Mwishoni mwa kumbukumbu upande wa kulia

D Mwishoni mwa kumbukumbu upande wa kushoto

E Baada ya majina ya waliohudhuria na wasiohudhuria

Swali hili lilitoka katika umahiri wa kutumia maandishi katika kuwasiliana kulingana na miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuandika kumbukumbu za mikutano kwa kuzingatia vipengele vya uandishi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu. Jedwali Na. 28 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 28: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C	D*	E	Mengineyo
Idadi ya watahiniwa	180,287	119,483	395,137	286,593	111,167	15,084
Asilimia ya watahiniwa	16.3	10.8	35.7	25.9	10.0	14

Jedwali Na. 28 linaonesha kuwa, watahiniwa 806,074 sawa na asilimia 72.7 walichagua kati ya vipotoshi A *mwanzoni mwa kichwa cha kumbukumbu,* B *katikati ya kumbukumbu kwenye ajenda za mkutano*, C *mwishoni mwa kumbukumbu upande wa kushoto* na E *baada ya majina ya waliohudhuria na wasiohudhuria*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *mwanzoni mwa kichwa cha kumbukumbu* walishindwa kuelewa kuwa kichwa cha kumbukumbu za mikutano kinataja mkutano ulikuwa unahusu jambo au kitu gani na si kuweka saini ya mwenyekiti. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *katikati ya kumbukumbu kwenye ajenda za mkutano* hawakuwa na uelewa kuwa sehemu hii hukaa ajenda zote za mkutano kwa kuorodheshwa bila kuwepo na saini ya mwenyekiti. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *mwisho wa kumbukumbu upande wa kulia* walishindwa kuelewa kuwa sehemu hii hukaa saini ya katibu wa mkutano ambaye ndiye anayeandika kumbukumbu za mkutano. Aidha, watahiniwa wengine walichagua kipotoshi *baada ya majina ya waliohudhuria na wasiohudhuria*. Walishindwa kuelewa kuwa baada ya majina hayo kinachofuata ni ajenda za mkutano, ambazo hazina saini ya mwenyekiti wa mkutano. Hivyo watahiniwa waliochagua vipotoshi hivi hawakuwa na umahiri wa kutosha juu ya uandishi wa kumbukumbu za mkutano.

Hata hivyo, watahiniwa 28,658 sawa na asilimia 25.9 walichagua jibu sahihi D *mwishoni mwa* kumbukumbu *upande wa kushoto*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kubaini vipengele vya uandishi wa kumbukumbu za mikutano. Watahiniwa waliweza kutambua kuwa saini ya mwenyekiti katika uandishi wa kumbukumbu za mkutano hukaa mwishoni mwa kumbukumbu upande wa kushoto.

1.2 SEHEMU B: Utungaji

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano (36 - 40) na yalihusu umahiri mahususi wa kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali na watahiniwa walitakiwa kutumia weledi na umahiri mkubwa waliokuwa nao kukamilisha tangazo walilopewa kwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku.

Swali lilikuwa kama ifuatavyo:

Kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku, jibu swali la 36 - 40 kwa kuweka kivuli katika herufi ya jibu lililo sahihi katika fomu yako ya kujibia ili kukamilisha tangazo lifuatalo.

A saa 5:00 asubuhi	B +255 222333767	C KUKATIKA KWA UMEME
D Limetolewa na meneja wa TANESCO	E Shirika la Umeme Tanzania	

Swali la 36: _____

Swali la 37: _____ wilaya ya Bagamoyo linapenda kuwatangazia wateja wake wote kuwa kutakuwa na tatizo la kukatika kwa umeme tarehe 13/8/2021 siku ya Jumapili, kuanzia **Swali la 38**: _____ hadi saa 9:00 mchana. Sababu ya kukatika kwa umeme ni matengenezo makubwa ya kubadili nyaya katika njia kuu ya umeme. Maeneo yote ya wilaya ya Bagamoyo yatakosa huduma ya umeme. Shirika linaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

Swali la 39: _____

Wasiliana nasi kupitia,

Swali la 40: _____

Katika kujibu maswali haya, watahiniwa walitakiwa kukamilisha tangazo kama ifuatavyo:

36	37	38	39	40
C	E	A	D	B

Uchambuzi wa kina wa majibu ya watahiniwa katika kila swali (36 - 40) ni kama ifuatavyo:

Swali la 36

Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha tangazo. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 29 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 29: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C*	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	40,868	46,816	721,213	104,980	176,974	16,924
Asilimia ya Watahiniwa	3.7	4.2	65.1	9.5	16.0	1.5

Jedwali Na. 29 linaonesha kuwa watahiniwa 721,213 sawa na asilimia 65.1 walichagua jibu sahihi C *KUKATIKA KWA UMEME*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa uandishi wa matangazo mbalimbali. Hivyo, waliweza kubaini kuwa kichwa cha matangazo huandikwa kwa herufi kubwa na yasizidi maneno matano.

Swali la 37

Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika Shirika lililotoa tangazo husika. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 30 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo**.**

Jedwali Na. 30: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C	D	E*	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	48,899	40,069	141,719	274,193	585,497	17,398
Asilimia ya Watahiniwa	4.4	3.6	12.8	24.8	52.9	1.6

Jedwali Na. 30 linaonesha kuwa watahiniwa 585,497 sawa na asilimia 52.9 walichagua jibu sahihi, E *Shirika la umeme Tanzania*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kubaini kuwa jibu hilo ndilo jibu sahihi kwa sababu huonesha Shirika ambalo limehusika kutoa tangazo ambalo ni Shirika la Umeme Tanzania katika swali husika.

Swali la 38

Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika muda ambao umeme utakatika. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 31 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 31: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A*	B	C	D	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	952,159	32,227	44,778	37,054	30,880	10,677
Asilimia ya Watahiniwa	86.0	2.9	4.0	3.3	2.8	1.0

Jedwali Na. 31 linaonesha kuwa watahiniwa 952,159, sawa na asilimia 86.0 walichagua jibu sahihi A *saa 5:00 asubuhi.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa kanuni na taratibu za uandishi wa matangazo, hivyo kuweza kuonesha muda ambao umeme utakatika kutokana na swali husika.

Swali la 39

Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika cheo cha aliyetoa tangazo. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 32 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

Jedwali Na. 32: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo

Chaguo	A	B	C	D*	E	Mengine
Idadi ya Watahiniwa	33,476	49,373	168,860	621,435	218,840	15,791
Asilimia ya Watahiniwa	3.0	4.5	15.2	56.1	19.8	1.4

Jedwali Na. 32 linaonesha kuwa watahiniwa 621,435 sawa na asilimia 56.1 walichagua jibu sahihi D *limetolewa na meneja wa TANESCO*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa taratibu za uandishi wa matangazo, hivyo kuweza kuonesha mhusika aliyetoa tangazo ambaye ni meneja wa TANESCO.

Swali la 40

Swali lilimtaka mtahiniwa kukamilisha tangazo kwa kuandika njia ya mawasiliano iliyotumika katika tangazo. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Kielelezo Na. 8 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Kielelezo Na. 8: *Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.*

Kielelezo Na. 8 kinaonesha kuwa watahiniwa 969,481 sawa na asilimia 87.5 walichagua jibu sahihi B *+255222333767*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika uandishi wa matangazo, hivyo kuweza kuelewa kuwa anuani au mawasiliano ya mtoa tangazo hutokea mwishoni katika tangazo.

1.3 SEHEMU C: Ufahamu

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano (41 - 45) kutoka katika umahiri wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyosoma. Mtahiniwa alitakiwa kutumia umahiri na weledi katika kusoma kwa makini hadithi na kuwelewa kisha kujibu maswali kutokana na hadithi hiyo. Ifuatayo ni hadithi waliyopewa watahiniwa.

> Hapo *zamani za kale kulikuwa na Mzee Beberu na familia yake. Mzee huyo alikuwa na mke na watoto watatu ambao ni Chandachema, Mahangaiko na Shida. Mama yao alikuwa anaitwa Chakupewa. Familia yao ilikuwa tajiri. Walikuwa na mashamba*

lukuki, nyumba tatu, magari matatu pamoja na miradi mbalimbali. Baada ya miaka mitano kupita afya ya Mzee Beberu ilianza kutetereka. Mzee huyo alianza kuugua maradhi kadha wa kadha baada ya kupata ajali ya gari wakati akitoka kukagua miradi yake.

Mzee Beberu alikaa kitandani kwa miaka takribani mitatu baada ya kugundulika kuwa alikuwa amevunjika uti wa mgongo. Hakuwa na uwezo wa kunyanyuka mwenyewe bila msaada wa mtu mwingine. Hatimaye, Mzee Beberu alikata kamba. Baada ya kifo cha mzee huyo, maisha yalianza kubadilika katika familia kwa kuwa na migogoro mingi. Mahangaiko na Shida wakaanza kuwa na tabia mbaya ya ulevi na waliuza mali za familia. Miezi sita baadaye, hali ya maisha ilizidi kuwa mbaya hususani pale mali zote zilipouzwa hadi nyumba waliyokuwa wakiishi na mama yao. Mahangaiko na Shida waliondoka na kwenda kusikojulikana.

Chakupewa na Chandachema walibaki wakiishi kwa shida. Siku moja Chandachema aliongozana na mama yake msituni kutafuta kuni. Wakati wakiwa njiani mvua kubwa ilinyesha. Chakupewa alikuwa haijui vyema njia iendayo msituni hivyo, ilimlazimu kuweka alama kwa kuchuma majani na kudondosha njiani huku mwanaye akiwa anamuangalia. Kabla ya kufika msituni, Chakupewa aligongwa na nyoka. Hivyo, Chandachema alilazimika kumbeba mama yake na kurudi naye nyumbani ili kumpeleka hospitali. Chakupewa alipelekwa hospitali na kupata matibabu, akapona. Hatimaye alirudi nyumbani na kuendeleza maisha yake ya kawaida. Aliwakumbuka sana watoto wake Mahangaiko na Shida. Huko walikokwenda, Mahangaiko na Shida walitumia pesa zote zikaisha hatimaye wakaishi maisha ya shida mno. Walijutia matendo yao wakarudi nyumbani na kumtaka radhi mama yao.

Swali la 41: Andika kichwa kinachofaa kwa hadithi uliyoisoma.

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini kichwa cha hadithi walichopewa. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Kielelezo Na. 9 kinaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 41.



Kielelezo Na. 9*: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.*

Kielelezo Na. 9 kinaonesha kuwa watahiniwa 639,795 sawa na asilimia 57.8 walijibu kwa usahihi. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kusoma hadithi waliyopewa na kuandika kwa usahihi kichwa cha hadithi. Watahiniwa hao waliandika kichwa cha hadithi kwa kutumia maneno yao yanayosadifu hadithi kwa usahihi. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika kichwa cha hadithi kama vile, *Maisha ya Mzee Beberu* wengine waliandika *Mzee Beberu*. Kielelezo Na. 10 kinaonesha jibu zuri la mtahiniwa aliyepata alama zote.


SWALI LA 41
Mzee beberu na familia yake

Kielelezo Na. 10: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 41.

Hata hivyo, watahiniwa 467,980 sawa na asilimia 42.2 walishindwa kubaini kichwa cha hadithi kutokana na kutokuwa na umahiri wa kutosha wa kusoma hadithi na kubaini mawazo yaliyomo. Watahiniwa hao waliandika kichwa cha hadithi kinyume na taratibu za uandishi kwa kuandika maneno zaidi ya matano. Wengine walitaja majina ya wahusika yaliyomo katika hadithi, na wengine walinakili maneno kutoka katika hadithi waliyosoma. Kielelezo Na. 11 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.


SWALI LA 41 Hapo zamani zakale kulikua mzee barubaru nafamilia yake

Kielelezo Na. 11: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 41.

Swali la 42: Mwandishi anamaanisha nini akisema “alikata kamba?”

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya nahau “kata kamba” kama ilivyotumika katika hadidhi aliyoisoma. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Kielelezo Na. 12 kinaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 42.



Kielelezo Na. 12: *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.*

Kielelezo Na. 12 kinaonesha kuwa, watahiniwa 950,044 sawa na asilimia 85.8 walijibu kwa usahihi. Watahiniwa hao waliweza kueleza maana ya nahau ”alikata kamba” kuwa ni kuaga dunia, kupoteza uhai na kufariki dunia. Majibu hayo yanadhihirisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu usomaji wa hadithi na kuelewa maudhui yaliyomo ndani yake. Kielelezo Na. 13. kinaonesha jibu zuri la mtahiniwa huyo aliyepata alama zote.


SWALI LA 42 Kukata kamba maana yake kufariki dunia.

Kielelezo Na. 13: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 42.

Hata hivyo, watahiniwa 157,731 sawa na asilimia 14.2 walishindwa kutoa maelezo sahihi kwa kuwa hawakuweza kutambua maudhui yaliyomo. Baadhi yao walionesha kukosa stadi za kusoma na kuandika, na wengine kutokuelewa hadithi, hivyo kushindwa kuandika maana sahihi ya nahau “alikata kamba”. Watahiniwa wengine walitoa majibu kinyume na matakwa ya swali. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana

ya *alikata kamba* kuwa ni *alikata tamaa.* Kielelezo Na. 14 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa maana kinyume na matakwa ya swali.


SWALI LA 42 Alikata tamaa

Kielelezo Na. 14**:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 42.

Swali la 43: Kwa nini Chakupewa alichuma majani na kudondosha njiani wakati wa kwenda msituni?

Swali hili liliwataka watahiniwa kutoa sababu za Chakupewa kuchuma majani na kuyadondosha njiani wakati wa kwenda msituni. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Kielelezo Na.15 kinaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 43.



Kielelezo Na. 15: *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.*

Kielelezo Na. 15 kinaonesha kuwa watahiniwa 493,097 sawa na asilimia 44.5 walijibu kwa usahihi. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa usahihi sababu za Chakupewa kuchuma majani na kudondosha njiani wakati wa kwenda msituni. Watahiniwa hao walitoa sababu kuwa, alikuwa hajui njia hivyo aliweka alama ili aweze kukumbuka njia wakati wa kurudi nyumbani kutoka msituni. Huu ni uthibitisho kwamba watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu hadithi waliyosomewa. Kielelezo Na. 16 kinaonesha jibu zuri la mtahiniwa aliyepata alama zote.



Kielelezo Na. 16. Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 43.

Hata hivyo, watahiniwa 614,678 sawa na asilimia 55.5 walishindwa kutoa sababu zilizomfanya Chakupewa kuchuma majani na kudondosha njiani wakati wa kwenda msituni. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa hadithi hivyo kuandika majibu yasiyokidhi matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa jibu ambalo lilionesha sababu ya kifo cha mzee Beberu. Kielelezo Na. 17 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi ya swali husika.

Kielelezo Na. 17**:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 42.

Swali la 44: Nini kilisababisha kifo cha Mzee Beberu?

Swali hili lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuelewa maudhui yaliyomo katika hadithi na kueleza sababu iliyosababisha kifo cha mzee Beberu. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Kielelezo Na. 18 kinaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 44.



Kielelezo Na. 18: *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.*

Kielelezo Na. 18 kinaonesha kuwa, watahiniwa 984,873 sawa na asilimia 88.9 walijibu kwa usahihi. Watahiniwa waliweza kuelezea sababu ya kifo cha mzee Beberu kuwa ni maradhi yaliyotokana na ajali ya gari na kuvunjika kwa uti wa mgongo. Kielelezo Na. 19. kinaonesha jibu zuri la mtahiniwa huyo aliyepata alama zote.


SWALI LA 44

Kitu Kilicho Sababisha Kifo cha mzee beberu ni alipata ajali ya gari wakati akitoka Kukagua miradi yake

Kielelezo Na. 19*:* Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 44.

Hata hivyo, watahiniwa 122,902 sawa na asilimia 11.1 walishindwa kutoa sababu ya kifo cha mzee Beberu. Watahiniwa hao walitoa majibu tofauti na matakwa ya swali, kama vile, “falasi”. Watahiniwa wengine badala ya kutoa sababu za kifo cha mzee Beberu, wao walinakili mstari uliopo kwenye hadithi unaoonesha kifo cha mzee Beberu. Kielelezo Na. 20 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali.


SWALI LA 44 Ha timaye mzee beberu alikata kamba.

Kielelezo Na. 20: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 44.

Swali la 45: Hadithi hii inatufundisha nini katika maisha yetu ya kila siku?

Swali hili lililenga kupima umahiri wa watahiniwa katika kubaini mafundisho yanayotokana na hadithi waliyosomewa. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Kielelezo Na. 21 kinaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 45.



Kielelezo Na. 21: *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.*

Kielelezo Na. 21 kinaonesha kuwa, watahiniwa 690,242 sawa na asilimia 62.3 walijibu kwa usahihi. Watahiniwa hao walikuwa na mawanda mapana ya kuelewa mafunzo yaliyomo kama vile, *tusitumie mali ovyo, kuwa na ushirikiano, kuomba msamaha unapokosea, majuto ni mjukuu, tuwe wavumilivu kwenye shida na raha, tutunze mali zetu* na *kutotumia mali vibaya*. Kielelezo Na. 22 kinaonesha jibu zuri la mtahiniwa aliyepata alama zote.


SWALI LA 45 Kna tufundisha kuwa na tabia njema.

Kielelezo Na. 22*:* Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 45*.*

Hata hivyo, watahiniwa 417,533 sawa na asilimia 37.7 walishindwa kuandika mafunzo yaliyopatikana katika hadithi. Baadhi yao waliandika majibu kama vile, *umuhimu wa maisha, ukipata kitu kipya usitupe cha zamani* na *chanda chema.* Majibu hayo hayakuwa na uhusiano na hadithi waliyosomewa. Kielelezo Na. 23 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika mafunzo yasiyoendana na hadithi aliyopewa.


SWALI LA 45
MAUTHA YA SHIDA

Kielelezo Na. 23: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 45.

2.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI

Umahiri uliotahiniwa katika somo la Kiswahili ni *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali*, kutumia *msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali, kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali, kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo*

alilolisikiliza, kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma na *kutumia msamiati katika kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali*. Uchambuzi unaonesha kuwa, umahiri uliokuwa na kiwango cha juu zaidi ulikuwa ni *kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza (76.1%),* ikifuatiwa na *kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma* (70.0%), *kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali* (68.2%), *kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali* (63.7%), *kutumia msamiati katika kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali* (61.3%) na ya mwisho ilikuwa *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali* ambayo ilikuwa na alama za wastani (57.8%). Muhtasari wa ufaulu kwa kila umahiri umeoneshwa katika Kiambatisho cha Pekee.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, maswali matatu yaliyotahiniwa kati ya maswali saba katika umahiri wa *kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza* yalijibiwa vizuri zaidi, nayo ni swali la 1 (91.6%), 4 (90.7%) na 2 (90.0%). Katika umahiri wa *kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma*, swali la 44 lilijibiwa vizuri zaidi na kuwa na ufaulu wa alama (88.9%). Aidha, swali la 20, 22 na 42 yalijibiwa vizuri sana ambapo kiwango cha ufaulu kilikuwa zaidi ya asilimia 80, yaani (81.2%), (88.4%) na (85.8%) mtawalia. Pia, katika umahiri wa *kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali* maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi ni swali la 38 (86.0%) na 44 (87.5%). Katika umahiri wa *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali* swali la 18 (85.5%) na 16

(86.8%) ndiyo maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi. Kwa ujumla wastani wa ufaulu wa umahiri katika somo la Kiswahili ni asilimia 66.1.

3.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa umahiri unaonesha kuwa wastani wa kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili mwaka 2021 ulikuwa mzuri (66.10%). Vilevile, uchambuzi huu umebainisha changamoto zilizowafanya watahiniwa kushindwa kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi. Miongoni mwa changamoto hizo ni; kushindwa kutambua matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu msamiati na aina za maneno. Changamoto nyingine ni kuchagua na kusiliba jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika kujibu maswali mbalimbali katika fomu za OMR.

4.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

(i) Ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika umahiri mahususi wa kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza walimu wanatakiwa kuwaongoza wanafunzi katika stadi za ufahamu wa kusoma, kusikiliza na kuelewa matini mbalimbali ili kukuza stadi ya hiyo.

(ii) Walimu wahakikishe wanafunzi wanaelewa umahiri wa kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali hususani katika kuandika matangazo. Mwalimu anaweza kutumia picha na magazeti yenye matangazo mbalimbali katika kufundishia.

(iii) Walimu wanatakiwa kutumia mbinu ya *bungua bongo*, *kazi mradi* na *maigizo* kwenye ufundishaji wa nahau, methali na vitendawili ili kuwajengea uwezo na weledi mkubwa wa kufahamu dhana hizo.

(iv) Katika kuongeza ufaulu katika umahiri mahususi wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma, walimu wawafundishe wanafunzi misingi madhubuti ya kusoma ili kuwajengea uwezo wanafunzi katika kutumia misamiati mipya katika lugha ya Kiswahili. Aidha, wanaweza kuwapa wanafunzi vifungu vya habari/hadithi vilivyopo katika vitabu vyao vya kiada na kuwapa maelekezo ya kusoma na kujibu maswali atakayoulizwa.

KIAMBATISHO CHA PEKEE

UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA UMAHIRI KATIKA PSLE 2021

01 Kiswahili

NA.	UMAHIRI	MTIHANI WA 2021			
		Ufaulu kwa kila Swali		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni
		Namba ya swali	(%) ya Ufaulu		
1.	Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza.	1	91.6	76.1	Vizuri
		2	90.0		
		3	53.8		
		4	90.7		
		5	67.6		
		6	68.8		
		7	70.3		
2.	Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma.	20	81.2	69.9	Vizuri
		21	50.5		
		22	88.4		
		41	57.8		
		42	85.8		
		43	44.5		
		44	88.9		
		45	62.3		
3.	Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali.	23	66.7	68.2	Vizurii
		24	57.7		
		25	78.9		
		26	88.7		
		27	73.2		
		28	44.1		

NA.	UMAHIRI	MTIHANI WA 2021			
		Ufaulu kwa kila Swali		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni
		Namba ya swali	(%) ya Ufaulu		
4.	Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali.	34	72.7	63.7	Vizuri
		35	25.9		
		36	65.1		
		37	52.9		
		38	86.0		
		39	56.1		
		40	87.5		
5.	Kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali.	29	59.5	61.3	Vizuri
		30	71.7		
		31	39.8		
		32	86.9		
		33	48.6		
6.	Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali.	8	39.4	57.8	Wastani
		9	47.8		
		10	70.5		
		11	51.3		
		12	47.7		
		13	74.3		
		14	53.0		
		15	43.0		
		16	86.8		
		17	35.5		
		18	85.5		
		19	60.6		